# WASIFU WA SHUGHULI YA MRADI

Namna ya kujenga utamaduni wa ujumuishi na ulinzi wa watoto wenye ulemavu majumbani na shuleni unavoongeza mahitaji ya elimu maalum Dodoma - Tanzania.



Kisedet
Help street children in Tanzania

VaCNets Virtual Hub

# JINA LA MRAD:

Usaidizi wa ufikiwaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu dodoma

# MHUTASARI:

Mwaka 2021, Kisedet ilafanya tathimini ya kina juu ya elimu jumuishi kwa watoto wenye ulemavu katika jiji la Dodoma.
Tathimini ilionesha kuwa watoto 947 wenye ulemavu mbali mbali kwa mfano, ulemavu wa viungo 67%, ulemavu wa akili 13%, ulemavu wa macho 1%, viziwi 6%, usonji 1%, kuongea 3% na ualibino 9%. Pia, ilionekana kwamba watoto wenye ulemavu 25% waliathirika na unyanyasaji.

**947**
Watoto wenye ulemavu mbali mbali

**67%**
Ulemavu wa viungo

**13%**
Ulemavu wa akili

**1%**
Ulemavu wa macho

**6%**
Viziwi

**1%**
Usonji


**3%**
Ulemavu kutokuongea

**9%**
Ualibino

Tathimini zaidi ilionesha kuwa kati ya watoto wenye ulemavu 30 umri kati ya miaka 4-6 waliotakiwa kujiunga na shule za msingi; ni 11 tu waliojiunga na elimu maalumu ambapo ni (37%), wakati 16 (53.33%) waliunganishwa na shule za msingi jumuishi. Mbaya zaidi utafiti uliofanywa na HAKIELIMU mwaka 2011 ulionesha kwamba watoto wenye ulemavu walioandikishwa mashuleni walikosa walimu wazuri na walikumbwa na unyanyapaa, na kukataliwa hivyo utafiti huo ulidhihirisha kuwa watoto hao wamekosa haki yao ya msingi ya elimu.

Kati ya Watoto wenye ulemavu

Umri 4-6 miaka




## CHANGAMOTO


- **Ukosefu wa muelimishaji mtaalam**
- **Unyanyasaji**
- **utengwaji**


Kutokana na tathimini hizo, Shirika la KISEDET kwa kushirikiana na Agata Smeralda kutoka Italia iliandaa na kutekeleza mradi wa miaka miwili (2) kwa Dodoma wenye lengo la kupunguza ukatili, unyanyasaji na ubaguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu. Mradi KISEDET na Agata Smeralda unatumia mbinu mbili ambayo ni ujumuishi wa jamii na kutembelea mashule.

Takwimu kutoka kwa Afisa ufuatiliaji na tathimini wa KISEDET baada ya miezi sita ya utekelezwaji juni 2022 zilionesha kuwa ujumuishi wa jamii na elimu juu haki za watoto wenye ulemavu uliongezeka, jamii kutambua haki za watu wenye ulemavu hasa haki ya Elimu. Uelewa wa jamii umesaidia watoto wenye ulemavu 87 (53 ni wasichana wenye shida ya akili na 34 ni wnye ulemavu wa viungo) wenye umri kati ya miaka 12-16 walibainishwa kupitia mikutano ya kijamii ambao wengine waliachwa majumbani huku wakikumbana na unyanyasaji lakini baada ya jamii kuelewa waliunganishwa na shule za awali na shule za msingi.

# DHANA:

Tathimini iliyofanywa na KISEDET 2021 kuhusu elimu jumuishi katika jiji la Dodoma ilifanya namba ya watoto wenye ulemavu kuwa 947 (535me, 412ke). Takwimu zaidi zilionesha kuwa watoto 236 (81me na 155ke) ilionesha 25% ya watoto wote wenye ulemavu walikuwa na aina tofautitofauti za ulemavu wakili kama vile uonihafifu na usonji. Wasichana wenye ulemavu walikumbwa na udhalilishaji wakingono, unyanyasaji mpaka 60% wasichana wasiojua kusoma kwa Dodoma wanaelimu ndogo kuhusu usafi na elimu ya uzazi, sababu inayochangia ukatili na unyanyasaji katika jamii. Zaidi ya yote, nusu ya watoto wenye ulemavu walikumbwa na ukatili ni wenye ulemavu wa Ngozi, ualbino, uoni hafifu.



# MAELEZO YA MRADI:

**Shughuli za KISEDET kusaidia watoto wenye ulemavu kufikia elimu na kuwatembelea shuleni kama ilivyoshauriwa na** *HAKIELIMU mwaka 2011 na kuoneshwa kwenye sera ya taifa ya elimu* ***2014.***



## Ushiriki wa jamii.

Njia ya ushiriki wa jamii ilikuwa imetumiwa na KISEDET katika hatua za awali na kuthibitishwa kuwa na ufanisi. Katika muundo wa watoto wenye ulemavu (*CWD*s), mbinu ya ushiriki wa jamii ilipitishwa kwa makusudi ili kuongeza kiwango cha ushiriki wa jamii katika kusaidia upatikanaji wa *CWD* kwenye Elimu Rasmi; kupunguza unyanyapaa nyumbani na shuleni; na kukomesha ubaguzi dhidi ya *CWDs*. Mbinu hiyo ililenga kuvuta hisia za wadau muhimu (wadau wa elimu, maafisa elimu , watendaji wa kata na wadau wa elimu ) wa mifumo ya kisheria na sera ya *CWDs* ili kutetea kwa ufanisi utekelezaji wa miongozo ya sera iliyopo juu ya haki za *CWDs*. KISEDET katika utekelezaji, huitisha kikao cha wadau kila robo ya mwaka (mara moja kila baada ya miezi 3) kwa mafunzo, majadiliano na/au vikao vya elimu. Masuala makuu ya mada yaliyojadiliwa na wadau muhimu ni pamoja na: -

1. Haki za watoto na sheria ya mtoto kwa kurejelea Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (UNCRC).
2. Jinsi ya kusaidia *CWD* na mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ili kuwawezesha kupata elimu ya awali na msingi.
3. Jinsi ya kushirikisha wadau wengine kwa ufanisi hasa viongozi wa jamii juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto ikiwa ni pamoja na kufafanua hatua zinazowezekana za jamii kuwalinda *CWD* dhidi ya madhara, unyanyasaji, na unyanyapaa; na kuhakikisha usawa wa kijinsia kwa *CWDs*.

Katika ushiriki mpana wa jamii, wadau wote walielekezwa juu ya mahitaji na haki za *CWDs* ili kuwawezesha kupata uelewa wa kina juu ya changamoto za *CWDs* na hivyo kutetea haki zao; haja ya kuimarisha mfumo wa utoaji haki ili kujumuisha sheria ndogo zinazozuia wazazi, na walezi kuwanyanyapaa; uandikishaji wa shule wa *CWDs* katika ngazi zote; na mazoea mabaya ya kitamaduni ambayo yaliyowazuia kupata elimu rasmi. Mwelekeo wa kijinsia juu ya haki za *CWDs* ulisisitizwa kwa kurejea vifungu vya usawa wa kijinsia katika mfumo wa kisheria wa Tanzania hasa sheria ya Mtoto (2009) na sera ya Elimu ya 2014. Azimio moja kuu kutoka kwa mfululizo wa ushiriki wa jamii lilikuwa agizo linalohitaji kufuatwa na shule na kaya zote kuandikisha *CWDs* katika elimu rasmi ambayo ilitekelezwa katika kata zote 41 za Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Matokeo yake, jumla ya wasichana wenye ulemavu 87 (wenye umri wa miaka 12-16), waliotambuliwa kupitia ushiriki wa jamii ambao hawakua shule waliweza kuandikishwa shuleni. Kati ya wasichana hao 87, 53 wenye changamoto ya akili waliandikishwa shule maalumu za awali wakati 34 wenye ulemavu wa viuongo waliandikishwa shule za msingi.

# ZIARA SHULENI:

Ziara za shule kwa upande mwingine hutumika kama hatua ya KISEDET kuelewa mazingira ya shule kwa watoto wenye ulemavu na kugawana maarifa juu ya haki za watoto na walimu, wasimamizi, wanafunzi na wafanyakazi wasiofundisha. Nyenzo kuu ya marejeo ya majadiliano ya walimu ilikuwa Sera ya Elimu ya Tanzania na UNCRC huku ikiwalenga walimu waliofikiri kuwa *CWD* hawastahili haki ya kupata elimu, kubadili mtazamo huo na kuwaonesha kuwa *CWD* ni watoto kama watoto wengine wenye haki ya kupata elimu maalum kwa wakati.

Ziara za shule kwa wafanyakazi wa KISEDET hufanywa kila wiki, na kila mwezi kufuatilia hasa mazingira rafiki shuleni kwa watoto wenye ulemavu; mahudhurio yao na maendeleo ya kitaaluma na kufuatilia vipindi vya stadi za maisha vilivyotolewa kwa watoto wenye ulemavu. Waelimishaji wa shule za awali na msingi waliopatiwa mafunzo na KISEDET walikuwa na jukumu la kutoa vipindi vya stadi za maisha ili kukabiliana na unyanyapaa na ubaguzi wa kijinsia kwa watoto wenye ulemavu katika mazingira ya shule na nyumbani pamoja na kuwawezesha watoto wenye ulemavu kufahamu jinsia zao.

Kwa ujumla, mradi katika utekelezaji wake ulilenga angalau kunufaisha watoto wenye ulemavu 100 kwa mwaka ndani ya kata 41 za Dodoma na viunga vyake.

| Mbinu na aina ya shughuli | Viashiria | Tathimini ya kabla, Octoba 2020 | Tathimini ya baada, Juni 2022 |
|---|---|---|---|
| **Ushirikishwaji wa Jamii** | Namba ya Watoto wenye ulemavu waliopata msaada wa saikolojia na mahitaji ya kijamii. | 8 | 25 |
| | Idadi ya wanajamii waliopatiwa mafunzo | 6 | 60 |
| | Idadi ya Watoto wenye ulemavu waliopatiwa vifaa saidizi | 2 | 11 |
| | Idadi ya Watoto wenye ulemavu waliopatiwa vifaa vya shule | 2 | 14 |
| | Idadi ya Watoto wenye ulemavu waliopatiwa mazoezi ya viungo. | 9 | 19 |
| | Idadi ya Watoto wenye ulemavu walioandikishwa shule maalumu. | 11 | 87 |
| **Ziara shuleni** | Idadi ya ziara | 3 | 12 |
| | Idadi ya vyoo vilivyojengwa | 0 | 6 |
| | Idadi ya mikutano iliyofanyika. | 1 | 12 |

# MATOKEO



## Msingi wa Ushahidi: Mchakato wa Tathimini

Matokeo Kutoka kwa afisa ufuatiliaji baada ya miezi sita ya utekelezwaji takwimu zilionesha mabadiliko chanya katika uandikishwaji wa watoto wenye ulemavu katika elimu maalumu shuleni na kuongezeka uelewa wa haki zao kwa wazazi/walezi na kwa watoto wenye ulemavu wenyewe.

1. Idadi ya *CWD* waliojiunga na elimu maalum ya awali iliongezeka kwa asilimia 12.6 kutoka 11 hadi 87.

2. Maoni ya Tathmini ya Uhamasishaji kutoka kwa walezi 150 waliohamasishwa juu ya thamani ya watoto wenye ulemavu walionesha kuwa wa 102 (68%) wamepunguza vitendo vinavyonyanyapaa *CWDs* na matibabu yasiyo sawa kwa misingi ya jinsia.

3. Uelewa juu ya haki za *CWDs* uliongezeka hasa juu ya haki zao hasa haki ya elimu, haki ya kushirikishwa, haki ya mahitaji ya mhimu (mavazi, upendo, makazi) na ulinzi sahihi.

4. Hatua za jamii juu ya ujumuishaji wa CWDs katika elimu kupitia uandikishaji zilivutia Serikali kuingilia kati ujenzi wa shule tatu za ziada za elimu maalum katika Manispaa ya Dodoma ambayo iliongeza idadi ya shule za elimu maalum kutoka 5 hadi 8 mwishoni mwa mwaka wa kwanza wa mradi.

# FUNZO LA MRADI

1. Ushiriki wa jamii ni chombo chenye nguvu cha uhamasishaji na utoaji wa elimu juu ya mahitaji na haki za watoto wenye ulemavu. Pamoja na jukumu la jamii katika kusaidia *CWDs* kupata elimu sahihi na matibabu ya haki. Ushiriki wa wadau mbalimbali ulikuwa sababu muhimu ya mafanikio katika mkakati wa ushirikishwaji wa jamii kwani uliwezesha ushiriki wa wadau muhimu wa elimu hasa maafisa elimu wa kata, watendaji wa kata na madiwani walioongoza mafunzo na uhamasishaji wa haki za watoto na kusisitiza haja ya kutekeleza sera ya elimu ya mwaka 2014 kama inavyotoa elimu kwa wote. Ushiriki wa moja kwa moja wa maafisa elimu wa kata na watendaji wa kata ulivutia ushiriki wa wadau zaidi huku idadi ya kata zinazowakilishwa katika mafunzo ikiongezeka kutoka 5 hadi 41 kwa mwaka mmoja.

2. Vitendo vya serikali na jamii ni vya kupongezwa na kuimarishawa. Chini ya mradi huu, jukumu la uongozi lililotekelezwa na maafisa elimu wa kata na watendaji wa kata lilivutia ushiriki wa zaidi ya

Wadau kutoka kata zote za Dodoma wanaosimamia lengo la mradi katika kata 5. Vile vile, juhudi za jamii juu ya uandikishaji wa *CWDs* katika shule rasmi zilivutia umakini wa serikali na hivyo serikali kujenga madarasa zaidi na kutoa vifaa maalum vya elimu ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuwezesha ujifunzaji mzuri kwa watoto wenye ulemavu.

3. Ziara za mara kwa mara shuleni kufuatilia ustawi wa watoto wenye ulemavu umepunguza kwa kiwango kikubwa unyanyapaa kutoka kwa wenzao na watu wazima katika mazingira yao; umeongeza kujithamini na kujiamini kwa watoto wenye ulemavu; na kuthibitisha dhana kwamba ulemavu sio kutokuwa na uwezo.

---

**Mwandishi: Wasifu huu umeandikwa na kumilikiwa na** KISEDET na kituo cha matokeo na maendeleo ya ugunduzi (IIDC)

**Marejereo:** Namna ya kujenga utamaduni wa ujumuishi na ulinzi salama wa Watoto wenye ulemavu nyumbani na shuleni kulivoongeza ufikiwaji wa elimu maalumu Dodoma, Tanzania (2022), KISEDET, Dodoma Tanzania.

Kwa taarifa Zaidi wasiliana nasi:


**KISEDET**
Plot 7 Block 53 Nduka Street,
Area A Chamwino Dodoma

P.O Box 379, Dodoma, Tanzania
+255 (0) 759 458 315
info@kisedet.org
www.kisedet.org